

USHAIRI: KUNGA ZA UTUNZI

KITHAKA wa MBERIA

Shabaha yangu katika makala hii ni kuzungumzia utunzi wa mashairi kutoka mkalaba wa matumizi ya lugha. Nania kuonyesha kunga mbalimbali za fasihi ambazo huipa lugha ya mashairi uzito wa maana, utamu na uwezo wa kunasa fikra za msomaji au msikilizaji.¹ Ingawaje ilhamu ya kutunga shairi inaibuka kutoka akilini mwa mtunzi, natumai kuonyesha kwamba mbinu na mizungu mbalimbali inayotumiwa na washairi ili kutekeleza amali yao, ni jambo wanaotaka kutunga mashairi wanaweza kulimudu kwa kufundishwa, kujifundisha au kwa kujumulisha yote mawili. Ni hamu yangu kwamba makala hii itakuwa ya manufaa kwa wale ambao wana kiu ya kutunga mashairi bali hawajui jinsi ya kukata kiu hiyo.

Baadhi ya mbinu za utunzi ambazo nitazungumzia humu zimeelezewa kwa matao ya viwango mbalimbali kwingineko. Kwa mfano, katika kitabu chake maarufu kitiwacho *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*, K. A. Abedi ameonyesha namna ya kupata umbo mwafaka la shairi la vina na mizani. Abedi aliutazama ushairi kutoka mkabala wa umbo tu. Ingawaje kitabu hicho kimekuwa kikitumiwa kama mwongozo wa utunzi wa mashairi, hakishughulikii mbinu za utunzi zinazohusu ujumbe ambao ndio kiini cha kazi yote ile ya kishairi. Baadhi ya waandishi wengine ambao wamezungumzia, kugusia au kutaja mbinu za utunzi ni M. H. Abdulaziz (1979), Muhamadi wa Mlamali (1980), Kineene wa Mutiso (1982), M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi (1984) na J. M. Mayoka (1984). Vilevile katika toleo la 16 la jarida la *Mulika* la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, kumeorodhesha kile kinachoitwa “Msamiati wa Muda wa Fasihi”. Kazi hizo zote haziridhishi kwa kutokuwa wa upana na kina. Natumai makala hii itanda na kuzama kuliko kazi hizo.

Miongoni mwa kunga za fasihi zinazotumiwa sana katika ushairi ni ile ijulikanayo kama JAZANDA. Jazanda ni ulinganishi wa kitu au jambo na kitu au jambo jingine. Vitu hivyo viwili ni sharti vifanane angalau kwa baadhi ya sifa. Sifa inayolingana baina ya vitu hivyo viwili ndiyo mshairi huwa amedhamiria kumulika katika ujumbe wake. Kwa mfano, katika mshairi ya kijamii, baadhi ya washairi huwalinganisha wanawake warembo na vitu kama vile lulu, ua, nyota au ninga. Katika muktadha huo, sifa ya mwanamke ambayo mshairi huwa amenuia ni kuvutia - sifa ambayo pia inapatikana katika lulu, ua, nyota na ninga.

Katika utenzi wa *Inkishafi*, Sayyid Abdalla Ali Nasiri anasema:

Suu ulimwengu bahari tesi

Una matumbawe na mangi masi

Aurakibuo juwa ni mwasi

Kwa kulla khasara ukhasiriye

Madhumuni ya mshairi katika ubeti huo ni kuonyesha sifa za ulimwengu. Sifa hizo zinadhihirika vizuri kupitia picha ya bahari inayoteta, yaani iliyoachafuka, hasa iwapo bahari hiyo pia ina matumbawe. Kwa kulinganisha ulimwengu na ‘bahari tesi’, na yenye matumbawe, mshairi amewasilisha vizuri sifa za ulimwengu kama mahali hatari kwa asiye na tahadhari.

Kama inavyoonekana katika ubeti wa hapo juu, ulinganishi wa kijazanda si wa namna wazi. Sifa inayounga pamoja ulimwengu na bahari haitajwi kwa namna wazi. Mshairi hasemi kwamnba ulimwengu ni hatari kama bahari iliyoachafuka na yenye matumbawe.

Kama ilivyo jazanda, TASHIBIHI ni ulinganishi wa kitu kinachozungumziwa na kitu kingine kinachofanana nacho. Ulinganishi wa kitashibihi unatafautiana na ule wa kijazanda kwa kuwa ni wa moja kwa moja na unatumia msamiati wa ulinganishi kama vile ‘kama’, ‘ja’, ‘mithili’ na ‘mfano’. Kwa mfano, tutakuwa tumetumia tashibihi tunaposema:

Kwa hasira iliyopanda

Janga la ndwele na matanga

Lilipiga kijiji kumbo

Kama wimbi la Ungama

Katika ubeti huo, maradhi yaliyosababisha vifo, yalishambulia vikali na kuangamiza kijiji mithili ‘Wimbi la Ungama’ lilivyoangamiza mji wa Ungama.

Mfano mwingine wa tashibihi unapatikana katika shairi la ubeti mmoja la Muyaka, ambamo mtunzi anasema:

Nipaziwe nipaziwe khabari zako mwandani

Nambiwe hivi nambiwe simba kulala shakani

Kunyak'ua kama mwewe nyamangwe kamla ndani

Firigisi na maini ndivyo apendavyo samba.²

Katika ubeti huo wa kimaumbo 'kunyak'ua' kwa mshairi kumefananishwa na kule kwa mwewe - ndege ambaye hunyakua windo kwa kasi.

Kunga nyingine ya utunzi ambayo hutumiwa na washairi ni ile ijulikanayo kama TASHIHISI. Tashihisi ni matumizi ya lugha ambapo kitu kisicho na uhai hupewa uhai na au mnyama asiye na hisia hupewa hisia kinyume na hali halisi ulimwenguni. Katika kilele cha shairi lake zuri liitwalo 'Usiniuwe', A. Abdalla anasema:

Uhai! Nakuliliya, wewe ndiye upendwaye

Uhai! Huna ubaya, yupi akutukiyaye?

A! Uhai niombeya, mamangu sema naye

Pengine atasikiya, asiniuwe mamangu.

Nawe Haki nisemeya, kwa dhati ya matamshi

Sema na kuniombeya, nihurumiwe niishi

Mamangu anioneya, anioneya bilashi

A! Haki nihurumiya, asiniuwe mamangu

Mauti! Nihurumiya, Mauti! Sinitukuwe

Lipi nilokukoseya? Hatuna vita mi nawe

Toba! Nisikitiya, nisalimisha na wewe

Magoti nakupigiya, simsikize mamangu

Katika beti hizo tatu, mshairi anazungumzia Uhai, Haki, Mauti na Toba. Kwa kawaida, binadamu huzungumza na binadamu wenzake kwani ndio wenye uwezo wa kuzungumza naye. Kwa kuzungumzia Uhai, Haki, Mauti na Toba, mshairi ameviinua vitu hivyo kutoka hali yake ya

kutokuwa na uhai na hisia na kuvipa uhai, hisia na uwezo wa kusikia na kuhurumia kama walivyo binadamu. Mshairi ametumia tashihisi katika beti hizo.

Kunga hiyo ya tashihisi imewehi kutumiwa na washairi wengi, akiwemo Sayyid Abdalla ambaye, katika Inkishafi, amesema:

Mvi wa Manaya ukawafuma
na kutubukia katika nyama
Pasiwe mwatami mwenye kuatama
Au mwamba: ani, yalikuwaye?

Ambapo Manaya au Mauti yamepewa sifa ya binadamu ya kutumia mishale.

Wakati mwingine washairi hutumia MAFUMBO. Wanaelezea jambo kwa kuzungumzia jambo jingine tofauti kabisa. Kwa mfano, mshairi anaweza kuelezea maovu ya wanyonyaji kwa kuzungumzia wadudu wanyonyao damu kama vile mbungo, chawa, kunguni, viroboto na mbu. Mshairi anaweza kuonyesha maangamizi ya dhalimu kwa kuelezea kishairi kuangamia kwa mnyama mkali kama vile simba, mbogo, kifarau au mamba.

Mafumbo huwatumikia washairi katika vipengele mbalimbali vya ushairi. Kwa mfano, katika ushiri wa kimapenzi, mtunzi anaweza kutumia fumbo au mafumbo kuelezea mambo ambayo huwa ni mwiko kuzungumziwa kwa lugha ya moja kwa moja. Kwa kutumia fumbo au mafumbo, mshairi atatimiza malengo yake bila kuhesabiwa kuwa mwenye lugha chafu. Katika shairi lenye kichwa cha 'Itakapokukutana' Muyaka alifumba:

Ai farasi na simba, wangiapo kwenda mbio
Hut'arakanya marimba, na kukutakuta nyayo
Na kunguruma ja mwamba, ukimbile utishao
Ai, mato na kioo itakapokuk'utana!

Asingelitumia fumbo kuelezea mambo hayo ya 'farasi na simba', Muyaka angeghashi fahamu zetu. Kwa kutumia fumbo, ameepekana na hatari ya kuudhi wasikilizaji au wasomaji wa shairi!

Utanzu mwingine wa maisha ambamo mara nyingi washairi hulazimika kutumia mafumbo ni siasa, hususa siasa tenge. Ni hatari kuwakasirisha wenye mamlaka na uwezo. Chambilecho E. Hussein:

Katika kumnyonyoa mwewe manyoya, inamlazimu mnyonyoaji atahadhari
na miparuzo yake.

Ili kuepukana na mikwaruzo y miewe, kozi na vipanga, washairi wenye nia ya kuwanyonyoa manyoya ndege hao, mara nyingine hulazimika kutumia mafumbo katika ushairi. Hivyo basi, katika *Sauti ya Dhiki*, A. Abdalla anasema:

Kuna mamba, mtoni metakabari
Ajigamba, na kujiona hodari
Yuwaamba, kwamba taishi dahari

Memughuri, ghururi za kipumbavu
Afikiri, hataishiwa na nguvu
Tababuri, hakika ni maangavu

Akumbuke, siku yake ikifika
Roho yake, ajuwe itamtoka
Nguvu zake, kikomoche zitafika

Mwandishi huyo ametumia mafumbo mengi katika diwani yake. Ni jambo la kutia moyo na thibitisho la thamani ya mafumbo katika ushairi kuona kwamba hakurejeshwa korokoroni.

Mbinu nyingine inayotumiwa na washairi ni TASWIRA. Taswira ni picha inayochorwa na mshairi katika akili ya msomaji au msikilizaji wa shairi. Picha hiyo husawiriwa kwa kutumia lugha. Katika *Inkishafi*, mtunzi anasema:

Au enga vumbi la muangaza

wakati wa yua likitepuza
Mwenda kulegema akilisoza
asione kitu ukishishiye

Au enga meto limetukapo
wakati wa jua lilinganapo
Mwenye nyota hwamba 'ni mai yapo'
Kayakimbilia akayatwaye

Chenda akaona mwako wa yua
mai alotaka akayatuwa
Asifidi yambo ila shakawa
ikawa mayuto yasimsiye

Beti hizo tatu zinatupa picha mbili, picha ambazo mshairi ameunda kwa lugha mwafaka ili kuendeleza maudhui yake. Picha ya kwanza inatolewa na ubeti wa 15, nayo ya pili imechorwa katika beti za 16 na 17.

Katika shairi la 'Jinamizi', E. Kezilahabi ameelezea utawala dhalimu kwa kutumia taswira ifuatayo:

Watu weusi na weupe
Mtumbwini walikuwa wamesimama, wametulia
Na fimbo ndefu mikonononi mwao,
Na macho yao wameyakazia majini
Samaki ambaye kupata hewa
Aliinua kichwa chake juu ya maji
Utawala wa chuma ulimtoboa fuvu

La kichwa na kutupwa mtumbwini.

Mshairi amechora picha imara, picha inayochanganya mazingira ya kijeografia na binadamu na vifaa vya shughuli za binadamu.

Wakati mwingine washairi huelezea mambo kwa namna inayoyapa mambo hayo sifa zilizovuka kingo za uhalisia. Wanapofanya hivyo, huwa wametumia kunga ya CHUKU. Katika shairi la ‘Imani ya Mwana’, S. A. Mohamed anakipa kilio wingi wa machozi hivi kwamba machozi hayo yanajaza kikombe! Anasema:

MWANA

Kwani mamangu u ng’ombe, au punda wa dobi?

Nakuuliza usambe, nayavunja madhehebi

Nalia chozi kikombe, uchungu wanisibabi

Kweli jaza ya kiumbe, ni madhila na mapigo?

Kwa kutumia chuku katika ubeti huo, mtunzi ameweza kuonyesha kilio kikubwa sana ambacho mwana analizwa na usumbufu unaopata mamake. Kwa kutumia chuku, mshairi ametilia mkazo hali isiyoridhisha ya maisha ya mwanamke katika ndoa.

Mfano mwingine wa chuku unapatikana katika ubeti wa 45 wa utenzi wa *Inkishafi*. Katika ubeti huo, mshairi anaonyesha tofauti ya hali mbili za watukufu wa Pate, yaani hali ya walipokuwa hai na nyingine ya baada ya kuaga dunia kwao. Anasema:

Sasa walaliya moya shubiri

pasipo zulia wala jodori

Ikawa miwili kutaathari

dhiki za ziara ziwakusiye

Shubiri, au kipimo cha umbali baina ya kidole cha gumba na kile cha kati, ni urefu mdogo mno na, katika ulimwengu halisi, maiti hawezi kuzikwa katika kaburi ndogo kiasi hicho. Hata hivyo,

mshairi amewazika watukufu hao wa siku za nyuma katika kaburi hizo ili kuonyesha jinsi utukufu wao ulivyofinyaa na kuwa si lolote si chochote.

Chuku ni namna mojawapo ya kutilia jambo mzazo. Hata hivyo, kuna namna nyingine za kutilia mambo mkazo bila ya kuvuka mipaka ya uhalisia. Napendekeza kwamba, mkazo ambao si chuku, yaani, usiotia jambo chumvi, tuuite MISISITIZO. Misisitizo ni ya aina nyingi katika ushairi. Kwa mfano, mshairi anaweza kusesitiza ukweli unaohusu wingi, uchache, udogo au ukubwa kwa kurudia kivumishi chenye sifa anayolenga. Katika wimbo mmoja wa Kiswahili waimbaji huimba:

Na wageni pindi wakifika
tuzo zao zote wakaweka
tumbi tumbi miongo miongo
limekuwa leo wazi lango
wakaola kikawa kisongo
na wafupi wakinyoya shingo
wakaketi juu ya ulilli
hawakuwa ambao hawali
wenye kula wakaramba bungo
wakashiba ya mtengotengo³

Katika wimbo huu wingi wa zawadi umesisitizwa kwa kurudiwa neno ‘tumbi’ ambalo laonyesha wingi. Waimbaji hawatosheki na kiwango hicho cha wingi. Wanatumia na kurudia neno ‘miongo’. Neno ‘miongo’ tayari linaonyesha wingi wa wingi kwani ni wingi wa ‘mwongo’. Hivyo basi, kitu kinapoelezewa kuwa ‘miongo miongo’ kinapewa wingi wa miongo kadha wa kadha. Tunapoweka ‘tumbi tumbi’ pamoja na ‘miongo miongo’ tunapata lundo kubwa sana la tuzo.

Mfano mwingine wa kurudia neno kwa lengo la kusesitiza unapatikana katika wimbo mwingine wa Kiswahili usemao:

Kimlisha akimrehemu

kimuonya yakele maozi
kimlisha tambuu ya Siu
na laini laini ya Ozi⁴

Katika wimbo huu, ubora wa tambuu ya Ozi unatiliwa mkazo kwa maneno ‘laini laini’.

Namna nyingine ya kusesitiza ni kurudia neno lile kwa lile mwanzoni mwa kila mshororo katika ubeti au hata katika shairi zima. Kwa mfano, katika shairi lenye kichwa ‘Owa’, Muyaka amelirudia neno ‘owa’ kila anapoanza mshororo. Vivyo hivyo, S. A. Mohamed ameanza kila mshororo wa shairi la ‘Kiza’ kwa neno ‘kiza’.

Namna nyingine ya msisitizo na ambayo hutumika sana katika ushairi wa Kiswahili ni pale ambapo mshairi hutumia mshororo ule kwa ule mwisho wa kila ubeti wa shairi. Mshororo wa aina hiyo hujulikana kama mkarara. Wakati mwingine, badala ya kurudiwa mshororo mzima, washairi hurudia sehemu mojawapo ya mshororo huo, aghalabu kipande kimoja.

Baadhi ya washairi, akiwepo Muyaka, wamewahi kutumia ‘to’ kwa lengo la kusesitiza jambo. Katika ubeti mmoja wa shairi la ‘Mgogoto wa Zamani’, Muyaka anashawishi:

Jifungetoni masombo, mshike msu na ngao
Zile ndizo zao sambo, zijile zatoka kwao;
Na tuwakalie kombo, tuwapigie hario!
Wakija tuteze nao, wayawiapo ngomani.

Katika neno ‘jifungetoni’ ‘to’ ina kazi ya kutilia uzito kule kujifunga masombo, yaani kujifunga vilivyo.

Katika lugha ya kawaida, kuna mafungu ya maneno yenye kazi ya msisitizo. Mafungu hayo ya maneno ni kama vile ‘daima dawamu’ ‘-eusi tititi’, ‘-eupe pepepe’ ‘dhahiri shahiri’, ‘alasisiri kasiri’, ‘shaghala bhaghala’, ‘hobela hobela’, ‘giza totoro’ (au ‘giza tororo’). Mshairi anaweza kutumia mafungu hayo ya maneno kama malighafi ya kujengea msisitizo katika shairi.

Washairi pia husisitiza jambo kwa kutumia ukinzani wa lugha. Katika shairi lake refu lijulikanalo kama ‘Jogoo kijijini’ E. Hussein anatuambia:

Lakini sikio
Lilikuwa sikio la kufa

Hasha
Asilani halikufa
Ingelikuwa sikio limekufa
Singelewa upepo pitao njia

La hasha! Sikio halikuwa limekufa! Ujembe huo unapewa uzito zaidi na mtunzi kwa kutanguliza habari inayokinzana na ujumbe wenyewe, yaani habari kwamba ‘lilikuwa sikio la kufa’

Si jambo lisilo la kawaida mshairi kuuliza swali huku akiwa tayari anajua jawabu la swali. Maswali ya namna hiyo hayanuiwi kutafuta habari kama yalivyo maswali mengine katika lugha bali hudhamiriwa kutilia mkazo ujumbe anaouwasilisha mshairi. Hiyo ndiyo kunga ya utunzi ijulikanayo kama BALAGHA. Tutakuwa tumetumia balagha iwapo, kwa kutaka kutilia mkazo kuondolewa mamlakani kwa nguvu watawala watawalao kwa mabavu tutauliza:

Nambieni enyi wajuzi
Marcos na Malacanang
Wangali chanda na pete
Au mhanga na nuru?

Tayari tunajua jawabu la swali hilo. Ingawaje siku za nyuma Marcos na ikulu ya Malacanang walikuwa chanda na pete, hivi sana wametengana mithili mhanga na nuru.

Sayyid Abdalla ametumia maswali mengi ya namna hiyo katika *Inkishafi*. Kwa mfano, anauliza:

Wapi wa Kiungu wajaza kumbi
na Mashekhe mema ya Ki-Sarambi
Walaliya nyumba za vumbi-vumbi
ziunda za miti ziwaaliye

Wa wapi ziuli wa Pate Yunga

wenye nyuso ali zenye mianga?

Wengiziye nyumba za tanga tanga

Daula na ezi iwaushiye

Mshairi tayari anajua waliko wakazi “wa Kiungu wajaza kumbi” na vile vile “ziuli wa Pate Yunga”. Si mwenyewe anatuambia waliko! Kwa hivyo, haulizi maswali hayo kwa kutaka habari bali anadhamiria kutilia uzito ujumbe anaoutoa katika utenzi.

Kunga nyingine ya utunzi ambayo hutumiwa na washairi ni ile ya MAJAZI. Matumizi ya majazi huwa ni pale ambapo mtu, kitu au pahali panapozungumziwa na mshairi, hupewa jina linalowakilisha sifa zake. Kwa mfano, katika shairi la “Mwanakupata” la S. A. Mohamed, mtunzi anahadithia kishairi, akisema:

Kanenda Mwihaja, kwake muhisani

Kwa mwenzi, ndugu wa zamani

Kamweleza haja, shida za moyoni

Kupata viroja nyingi nukusani

Kwa Mwanakupata

MWIHAJA

Kanena: “Pulika, rafiki amini

Mimi nadhilika, nimo mashakani

Niafu haraka, niwe sitarani

Hifadhi nataka, hebu niauni

Ni wa madaraka”

MWANAKUPATA

“Siwezi ondoka, sikwelewi sini

Wapi unatoka, kakuleta nani?

Hamwishi kutaka, nyinyi masikini
Upesi toweka, siye asilani
Ondoka! Ondoka”

Katika beti hizo tatu, tuna wahusika wawili, Mwihaja na Mwanakupata. Kila mmoja wa wahusika amepewa jina linaloonyesha hali yake ya kiuchumi. Mwihaja ni dhalili mwenye haja. Naye Mwanakupata ni tajiri aliyepata mali. Majina ya wahusika hao wawili yana maana na madhumuni maalum katika shairi; ni majina ya kimajazi.

Wakati mwingine, katika kuelezea habari fulani, mshairi hutoa nafasi kwa mtu au kitu kinachohusika kuzungumza chenyewe. Mshairi anapofanya hivyo, yaani anapoyanukuu maneno halisi yaliyosemwa, huwa anatumia mbinu iitwayo LITIFATI. Tuchukue mfano:

Alizoazoa nia
Akatunisha kifua
Akakaza misuli
Na kwa sauti ya chuma
Akakamea Mauti
Ngo! Siendi!
Siendi kaburini!

Katika ubeti huo, badala ya anayehadithia kuelezea jinsi nia imara ya kuishi ya mgonjwa mahututi ilivyopiga vita kifo kilichotaka kumburura, amemwachia mgonjwa huyo nafasi aelezee alivyopigana. Mhadithiaji amenukuu moja kwa moja maneno yaliyotolewa akilini, yaani, nia ya mgonjwa ya kuishi.

Katika shairi la “Utavaa Nguo Gani”, Muyaka anasema:

Nalikwambia “Sitende”, ukanambia “T’atenda!”
Iwe mwana usenende, ukanambia “T’akwenda!”
Leo u mvundevunde, ufuamile kitanda

Kesho wenzi washinda, utavaa nguo gani?

Katika ubeti huo, Muyaka amenukuu alichokisema msemaji katika shairi na kilichosemwa na aliyekuwa akitolea nasaha. Maneno halisi yaliyosemwa yanatufikia katika hali ya nafsi ya kwanza. Hivyo ndivyo hutumiwa litifati, habari hufikishwa kwa msomaji au msikilizaji wa shairi ikiwa katika nafsi ya kwanza. Hivyo basi, tunaposoma Inkishafi, tunasikiza sauti ya dunia ikiamrisha baada ya kukoma sauti ya msemaji katika mshairi:

Tandi la mauti likawakota

wakauma zanda na kuiyuta

Na dunia yao ikawasuta

ichamba: Safari! Muniukiye!

Katika shairi linalosimulia kisa au visa, mshairi anaweza kutumia TAASHIRA. Taashira huwa imetumiwa pale ambapo mtunzi ameelezea jambo kwa kutaka kuashiria jambo jingine muhimu litakalofuata katika mkururo wa mambo. Kwa mfano, mshairi anaweza kutumia mlio wa bundi kuashiria kifo. Vivyo hivyo, wekundu wa anga, kwa mfano, unaweza kutumiwa kama ishara ya umwagikaji wa damu.

Baadhi ya washairi huchanganya lugha ngeni na lugha wanayoitumia kutungia shairi. Aghlabu, washairi hufanya hivyo wanapodondoa maandishi mengine yaliyoandikwa kwa lugha ya kigeni. Mbinu hiyo ya utunzi inajulikana kama TADMINI.⁵ Muyaka ni miongoni mwa washairi ambao wamewahi kutumia tadmini katika ushairi. Kwa mfano, alifanya hivyo katika beti zifuatazo:

Ilhali wa Maulaya, Sayyidi wa Sayyidahu

Naomba hinyenyekeya ya Rabbi afuwahu

Mawi Ngatubaidia yaliyo na ikrahu

“Faqadarnahu, fa nii ‘malqadiruna

Fa kam li n’ nabii waliopita radahu

Ambao wali wenyii, Musa na Isa na Nuhu

Mbona hawakujidai, wakamba ‘Dunia ndehu’?

“Faqadarnahu, fa nii ‘malqadiruna

Katika beti hizo mbili Muyaka ametumia maneno mengi ya Kiarabu katika shairi la Kiswahili.⁶

Katika *Inkishafi*, Sayyid Abdalla alitumia jazanda aliposema:

Dunia jifa siikaribu

Haipendi mtu ila kilabu

I hali gani, ewe labibu

Kuwania na mbwa hutukizwaye?

Muyaka alitumia jazanda inayolingana na hiyo aliposema:

Ai ulimwengu jifa, dunia ya makhaini

Iliyo t’ule sifa, isokoma nukusani

Humwangusha msharafa, akapomoka kwa tani

Ikamwondoa kitini, kwa mato achangalia

Katika beti hizo mbili, Sayyid Abdalla na Muyaka wametumia jazanda iliyomo katika methali ya Kiarabu inayosema “Al-dunya jifa la yuhibbuhu ila I kilabu”, yaani, dunia ni mzoga huvutia majibwa peke yao.⁷

Mshairi anaweza kutumia MLIO-ISHARA / TANAKUZI-SAUTI. Lugha zina milio ambayo hufanana na vitu au hali mbalimbali ulimwenguni. Milio hiyo huwa kama ishara ya kile kinachoshabihishwa nayo. Kwa mfano, ng’ombe hulia ‘ngo-o! ngo-o!; miguu ya watu wanaokimbia hulia ‘kum! Kum!; ngoma ya msondo hulia ‘tum! tum!’, nao baadhi ya ndege huruka ‘bru! bru!’ kutoka utanzu mmoja wa mti hadi utanzu mwingine. Mshairi anaweza kutumia milio kama hiyo kwa minajili ya kuyaimarisha maelezo ya kile ambacho husimamiwa na mlio. Kwa mfano, katika shairi la “Usiniuwe”, A. Abdalla ametumia mbinu hiyo ya mlio-ishara kukiimarisha kilio cha mtoto. Mbinu hiyo pia imetumiwa katika dondoo lifuatalo:

Nilikuona ulivyokuwa

Baada ya fahamu zako

Kupiga mbizi kali
Bwawani mwa ghamu-
Mashaka na dhiki
Ngozi na mifupa
Nakumbuka ulivyotamba
Huku machozi mekundu
Yakidondoka ndo! ndo! ndo!
Mithili matone ya zahama
Majira ya shakawa⁸

Wakati mwingine washairi hutumia sehemu ya kitu kuwakilisha kitu kizima. Ningependa kuiita kunga hiyo SEHEMU-WAKILISHI. Sehemu hiyo inaweza kuwa ya mwili, mti, kifaa au mfumo fulani. Kwa mfano, katika shairi la E. Hussein liitwalo “Ngoma na Vailini” ambalo, kama anavyosema M. H. Abdulaziz (1979:104), linahusu hali ya utata inayotokana na mgongano wa tamaduni, mtunzi ametumia ‘ngoma’ kuwakilisha utamaduni wa mwafrika na ‘vailini’ kuwakilisha utamaduni wa mzungu. Kama ala ya muziki, ngoma imekuwa ikitumiwa na ingali inatumiwa na makabila mbalimbali ya kiafrika katika sherehe na ngoma mbalimbali. Nayo vailini hutumiwa katika nyimbo za kizungu. Mhusika au msemaji wa “Ngoma na vailini” anafikiwa au kujiwa na sauti kutoka ala zote mbili kwani yumo kwenye makutano ya tamaduni zote mbili. Vilevile katika shairi hilohilo, mshairi ametumia kanzu kuwakilisha mfumo wa Kiislamu na msalaba kuwakilisha mfumo wa Kikristo.

Baadhi ya washairi hutumia IMANI za jamii na vilevile HADITHI ZA VISA VYA KIHISTORIA.⁹ Turejelee ubeti tulioutoa awali unaosema:

Kwa hasira na mori
Janga la ndwele na matanga
Lilipiga kijiji kumbo

Kama wimbi la Ungama.

Tashibihi ya ubeti huo imejengeka katika msemu wa “Humuwezi kwima, liushalo wimbi Ungama”. Kwa upande wake, msemu huo umetokana na imani miongoni mwa baadhi ya Waswahili kwamba hapo zamani za kale ulikuwepo mji mmoja uliojulikana kama Ungama, ambao uliangamizwa na Mungu kwa kutumia wimbi la bahari. Inasemekana kwamba Mungu alikasirishwa na kiburi cha wakazi wa mji huo, ambao kwa sababu ya utajiri wao wa hali ya juu sana walikuwa wakioga kwa maziwa badala ya maji (J. Knappert, 1979).

Hizi ni baadhi ya kunga muhimu za utunzi zinazowafaa sana washairi katika kipengele cha maana, kipengele ambacho ni muimu katika shairi lolote lile. Hizo ndizo kunga ambazo hujenga maudhui na ujumbe wa shairi na vilevile kulipa umbo lake la ndani. Katika sehemu ya makala hii iliyosalia, ningependa tutizame kunga za utunzi ambazo hulipa shairi umbo la nje.

Kufikia hivi leo (1987) mashairi mengi ya Kiswahili ni yenye vina na mizani. Hivyo ndivyo ulivyo ushairi wa washairi kama vile Ali Koti, Mwalimu Sikujua, Sayyid Abdalla bin Ali bin Nasir, Muyaka bin Haji, Shaaban Robert, Mathias Munyapala, Ahmed Nassir, Sadaan Kandoro, Abdilatif Abdalla na Hassan Mwalimu Mbega. Tutizame namna watunzi hao na wengine wengi wa mkondo huo wa ushairi wanavyofaulu kuyapa mashairi yao umbo tunalolijua.

Mojawapo ya kunga za utunzi zinazolipa shairi umbo la nje ni ile ijulikanayo kama INKISARI. Inkisari ni ufundi utumiwao na washairi kufupisha mishororo ya mashairi pindi wagunduapo kwamba wasipofanya hivyo, mishororo hiyo itakuwa mirefu kuliko mishororo mingine ya shairi, hali ambayo hulipa shairi linalohusika uguni. Namna mojawapo ya inkisari ni kuunga pamoja maneno mawili baada ya kuondolea mbali baadhi ya sauti za mojawapo ya maneno hayo. Hivyo basi, tukiwa na mshororo wa mizani kumi na saba katika shairi ambapo lengo letu ni kuwa na mizani kumi na sita, tunaweza kupunguza mizani hiyo hadi kumi na sita kwa kuunga pamoja maneno mawili. Ikiwa, kwa mfano, mshororo ulio na mizani kumi na saba una maneno ‘pahali pake’, tunaweza kuunga pamoja maneno hayo mawili na kupata neno moja ‘pahalipe’. Katika ‘pahali pake’ tuna mizani mitano ilhali katika ‘pahalipe’ tuna mizani minne. Hivyo basi, tutakuwa tumepunguza mizani moja, jambo ambalo litafupisha mshororo unaohusika kutoka mizani kumi na saba hadi kumi na sita na, kwa hivyo, kuzuia uguni katika shairi hilo. Katika shairi la ‘Usiniuwe’, A. Abdalla ametumia ufundi huo anaposema:

Tone lilipoanguka, mahalipe maalumu
Hapo likahifadhika, kungoja muda utimu
Kisha likabadilika nikawa pande la damu
Wata roho kunipoka, mamangu nihurumiya

Katika ubeti huo mshairi ametumia ‘mahalipe’ badala ya ‘mahali pake’ na vile vile ‘mamangu’ badala ya ‘mama yangu’.

Kwa kutumia mbinu hiyo tunaweza kuunda, kwa mfano, ‘zamuye’, ‘babake’, ‘nduguze’ na ‘dadao’ badala ya ‘zamu yake’, ‘ndugu zake’ na ‘dada yao’ mtawalia. Kama mifano tuliyoitoa inavyodhihirisha, maneno ambayo huungwa pamoja aghlabu huwa ni nomino na kivumishi hususa kivumishi cha umiliki.

Namna nyingine ya inkisari ni pale ambapo mshairi hupunguza mizani ya neno bila kuliunga pamoja na neno jingine. Turejeele shairi la ‘Usiniuwe’. Katika ubeti mmoja wa shairi hilo mtunzi ameandika:

Bado sijakamilika, halijesha umbo langu
Sitakwisha kwa haraka, zitapita siku tungu
Huna haki kunipoka, uhai ni haki yangu
Niwata takamilika, mamangu nihurumiya.

Licha ya mtunzi kutumia inkisari ya kuunga pamoja maneno mawili katika ‘mamangu’, pia ametumia inkisari ya aina ya pili. Badala ya kusema ‘nitakamilika’ mshairi amefutilia mbali ‘ni’ na kusema ‘takamilika’. Kwa kutumia inkisari za aina zote mbili katika mshororo wa nne, mshairi amefaulu kupunguza mizani kutoka kumi na minane hadi kumi na sita kama ilivyo mishororo mingine ya ‘Usiniuwe’.

Kwa kutumia inkisari ya kufupisha neno bila kuliunga pamoja na neno jingine, tunaweza kuunda, kwa mfano, ‘siende’ au ‘sende’ kutoka ‘usiende’. Vivyo hivyo, tunaweza kuunda ‘wasopenda’ (au hata ‘sopenda’) kutoka ‘wasiopenda’, ‘liso’ kutoka ‘lisilo’, ‘pasi’ kutoka ‘pasipo’, ‘takwenda’ kutoka ‘nitakwenda’ na ‘sendi’ kutoka ‘siendi’. Ingawaje kuna namna

mbalimbali za kufupisha maneno, aina inayotumiwa sana ni ile ya kuondolea mbali kiambishi kitangulizi kinachosimamia nafsi katika kitenzi.

Mbinu nyingine inayotumiwa katika ushairi wa vina na mizani ni ile itwayo MAZIDA. Mazida ni uongezaji wa sauti katika maneno. Zipo namna mbalimbali za kufanya hivyo. Kwa mfano, mshairi anaweza kuongeza vokali (au irabu) katika neno, jambo ambalo litaongeza silabi na, kwa hivyo, mizani katika neno hilo. Kufanya hivyo husababisha kurefuka kwa mshororo unaohusika. Matokeo ya ufundi huo ni kupata, kwa mfano, ‘muwili’ kutoka ‘mwili’, ‘muwaka’ kutoka ‘mwaka’ na ‘muwezi’ kutoka ‘mwezi’. Mazida ya hii inatumiwa pale ambapo mshairi amepungukiwa na mizani katika mshororo. Ikiwa, kwa mfano, katika shairi la mizani kumi na sita kila mshororo, mshairi amekabiliwa na tatizo la kuwa na mshororo ulio na mizani kumi na tano na akagundua kwamba mshororo huo una neno ‘mwongo’ (yaani, miaka kumi), mshairi atakuwa na mzungu mzuri wa kuepukia uguni kwa kutumia ‘muwongo’ badala ya ‘mwongo’. Kufanya hivyo kutarefusha neno hilo kutoka mizani miwili hadi mitatu, jambo ambalo lisababisha kurefuka kwa mshororo mzima kutoka mizani kumi na tano hadi kumi na sita.

Mshairi anayeelewa vyema fonolojia ya Kiswahili anaweza kurefusha mshororo wa shairi kwa mazida ya kurejesha maneno katika hali yake asilia ya kifonolijia; yaani hali ambayo bado haijaathiriwa na sheria za kifonolojia. Hivyo basi, mshairi anaweza kutumia ‘kiuma’ badala ya ‘chuma’, ‘kiumba’ badala ya ‘chumba’, ‘kiama’ badala ya ‘chama’, ‘kiombo’ badala ya ‘chombo’ au hata ‘kia’ badala ya ‘cha’. Kufanya hivyo huongeza mizani katika neno linalohusika na, kwa hivyo, kurefusha mshororo lilimotumiwa hilo neno.

Mazida ya aina nyingine ni ile ambayo haiongezi mizani katika neno wala kurefusha mshororo bali humpa mshairi kina anachotaka. Tutizame ubeti ufuatao wa shairi liitwalo ‘Imani ya Mwana la S. A. Mohamed’:

Sitasakamwa kauli, nikaumiza umiyo

Nikabeba idhilali, nikautweza na moyo

Siuwati ukweli hazidisha gugumiyo

Baba hafanyi halali, nawe hwachi vumiliyo

Hebu nambie

Kweli jaza **ya** kiumbe, ni madhila na mapigo?

Katika ubeti huo, mtunzi amebadilisha maneno ‘umio’, ‘gugumio’ na ‘vumilio’ na kuyafanya ‘umiyo’, ‘gugumiyo’ na ‘vumiliyo’ mtawalia. Jambo hilo halibadilishi idadi ya mizani katika maneno hayo. Kwa mfano, ‘umio’ na ‘umiyo’ ni maneno yenye mizani mitatu kila moja. Vivyo hivyo, ‘gugumio’ na ‘vumilio’ kwa upande mmoja na ‘gugumiyo’ na ‘vumiliyo’ kwa upande wa pili, ni maneno yaliyo na mizani minne kila moja. Shabaha ya mageuzo hayo ni kumpa mshairi kina cha nje cha ‘yo’ katika mshororo wa kwanza, wa tatu na wan nne, hali ambayo imefanya vina vya mshororo hiyo kuwiana na kina cha mshororo wa pili ambapo tuna neno ‘moyo’. Hivyo basi, kwa kutumia mazida hiyo, mtunzi ametimiza lengo lake la kuwa na ‘yo’ kama kina cha nje katika ubeti huo. Mshairi amefanya hivyo kwa kuongeza kiyeyushi (nusu vokali) ‘y’ kabla ya vokali ‘o’ katika kila mojawapo ya maneno matatu yanayohusika.

Mbali na kutumia inkisari na mazida, mshairi pia anaweza kuepukana na uguni wa wingi au uchache wa mizani kwa kutotumia neno alilodhamiria pindi agunduapo kwamba litazidisha au kupunguza mizani ya mshororo na badala yake akatumia neno mwafaka kimizani na ambalo linalingana na neno la kwanza kimaana. Mshairi anapotumia ‘ndwele’ badala ya ‘maradhi’ au ‘ugonjwa’ atakuwa amepunguza mizani ya mshororo unaohusika. Kinyume chake, yaani kutumia ‘maradhi’ au ‘ugonjwa’ badala ya ‘ndwele’ kutamwezesha mshairi kuongeza mizani. Kuna maneno katika lugha yanayolingana au kukaribia kulingana kimaana. Kwa mfano, tuna maneno kama vile ‘dhiki’, ‘mashaka’, ‘shakawa’ na ‘zahama’; ‘kisa’ na ‘kituko’; ‘kidole’ na ‘chanda’; na ‘rafiki’ na ‘sahibu’. Pia kuna maneno mengine yenye sura mbili za kifonolojia na ambazo hutofautiana kwa urefu. Mifano mizuri ya maneno kama hayo ni ‘mwanga’ na ‘mwangaza’; na ‘jaa’ na ‘jalala’. Mshairi anaweza kutumia mojawapo ya sura hizo mbili za neno moja kulingana na uhitaji wake katika shairi.

Kunga nyingine ya utunzi ni ile ijulikanayo kama TABDILA. Tabdila ni kubadilisha vokali iliyo mwisho wa kipande kwa lengo la kupata kina mwafaka. Katika shairi la ‘Kiswahili’, A. Nassir anasema:

Kiswahili nakutuma, lugha njema ya maani

Tukuwa hizi nudhuma, utangaze duniyani
Asojua kukusema, umfunze kwa makini
Apate kukibaini, kinenwavyo Kiswahili.

Mtunzi ametumia ‘maani’ badala ya ‘maana’ ili apate kina cha ‘ni’. Amefanya hivyo kwa kubadilisha vokali ya mwisho kutoka ‘a’ hadi “i”. E. Hussein ametumia ufundi huohuo katika shairi lake la ‘Jogoo Kijijini’. Ameandika:

Ndiyo maani
Wale watu wa ndani
Kifo wakajitazamia

Mtunzi ametumia ‘maani’ kwa maana ya ‘maana’ ili kupata ‘ni’ inayooana na ‘ni’ ya ‘ndani’.

Badala ya mshairi kubadilisha vokali ya mwisho katika kipande ili kujipatia kina anachohitaji anaweza kubadilisha mpangilio wa maneno katika kipande au mshororo mzima hivi kwamba neno linaloishia na kina anachotaka linakuja mwisho wa kipande kinachohusika. Huo ndio ujuzi uliotumiwa na A. Nassir katika shairi la ubeti mmoja liitwalo ‘Fimbo ya Mbali’, ambamo mshairi anasema:

Ufungapo zako tambo, zifunge kwa taamuli
Kwa viliwaza vya umbo, kattu sipige ramli
Nyoka kwa ya mbali fimbo, kufa haijawa kweli
Usipoteze akili, tenda watu watendayo.

Kwa mujibu wa sheria za sarufi ya Kiswahili, nomino hutangulia kivumishi au vivumishi katika fungu nomino. Hivyo basi, tunasema, kwa mfano, ‘tambo zake’ na ‘mtoto mmoja mwembamba’. Katika ubeti tulioudondoa hapo juu, mshairi amebadilisha mpangilio wa kisarufi hivi kwamba anasema ‘zako tambo’ badala ya ‘tambo zako’ na pia ‘ya mbali fimbo’ badala ya ‘fimbo ya

mbali’ (kama ilivyo katika kichwa cha shairi). Mageuzo hayo ya mpangilio wa maneno yamefaulu kumpa kina cha ndani cha ‘mbo’ katika mshororo wa kwanza na wa tatu.

Mbinu ya mwisho nitakayozungumzia humu ni TAKRIRI. Sauti moja au sauti tofauti bali za nasaba moja ya kifonolojia zinaporejelewa katika mshororo au mishororo kadhaa hutia shairi utamu. Hali hiyo hutekelezwa kwa kutumia takriri. Hiyo ndiyo mbinu niliyotumia katika shairi langu liitwalo “Wazo kwamba Uwe Pete”;

Wazo kwamba uwe pete
Pete azizi ya feruzi
Au ya almasi pendezi,
Nami kidole kiteule
Ambacho kipetwe ni pete,
Hiyo ni mbingu ya makungu
Iliyotanda adabu ya dhahabu,
Ni uwanda wa mijakaranda
Katikati ya Oktoba,
Ni asubuhi ya asumini
Dirishani mwa maisha
Ni nuru ya lulu
Chini ya macho ya moyo.

Natumai msomaji anaona ninachomaanisha ninaposema kwamba nimetumia takriri katika shairi hilo.

Turejeele ubeti juu ya “janga la ndwele”:

Kwa hasira na mori
Janga la ndwele na matanga
Lilipiga kijiji kumbo

Kama wimbi la Ungama

Ubeti huu umetumia kunga mbalimbali za utunzi kwa pamoja. Umetumia tashihisi - janga la ndwele lina hasira na mori; umetumia msisitizo - janga la ndwele linaandamana na matanga (linasababisha vifo); umetumia tashibihi - janga la ndwele lina uwezo wa kuangamiza kama wimbi la Ungama; na mwisho, ubeti huo umetumia imani ya jamii - imani kwamba zamani ulikuwako mji wa Ungama ulioangamizwa na wimbi la bahari. Kwa maoni yangu, kutumia kunga kadhaa katika huo huo kunaupa uzito zaidi wa kishairi. Mbali na kujua kutumia kunga mojamoya ni bora zaidi mshairi anapojua, sio tu kuzichanganya pamoja katika shairi, bali pia katika ubeti mmoja. Jambo muhimu sana, ni kujua kuzichanganya kwa namna inayoleta ufungamano na utangamano mzuri wa maana.

Naonelea tutue hapa. Nimejitahidi kadiri uhalisi wa mambo ulivyoniruhusu. Nasema ‘kadiri uhalisi ya mambo ulivyoniruhusu’ kwani nimekuwa nashughulikia mada ambayo inahitaji kuchunguzwa katika upana wa kitabu badala ya makala. Ijapo nalitambua jambo hilo, pia naamini kwamba makala hii imezitalii zile kunga ambazo, kwa maoni yangu, ndizo muhimu sana katika utunzi wa mashairi. Baadhi ya kunga hizo, kama vile ‘tashihisi’ na ‘tashibihi’ tayari zina majina. Nyingine kama vile jazanda na chuku zina majina zaidi ya moja. Hivyo basi, kwa baadhi ya watu jazanda hujulikana kama ‘istiari’ nayo ‘chuku’ huitwa ‘iblagh’. Nilipojikuta katika hali kama hiyo nilichagua kutumia mojawapo ya majina mawili yanayotumika. Kwa maoni yangu, kile ambacho ni muhimu zaidi si kutumia istilahi hii au ile bali kufahamu vyema matumizi ya lugha yanayohusika. Kuna mbinu nyingine za utunzi ambazo yumkini hazina majina maalum yanayokubalika. Nilipojikuta katika nyanda kama hizo, nilionelea nipendekeze istilahi za kutumia wakati wa kuongelea matumizi hayo ya lugha. Hivyo basi, nimependekeza istilahi kama vile ‘mlio-ishara’ na ‘sehemu-wakilishi’.

Ni matumaini yangu kwamba makala hii itakuwa na manufaa mbalimbali. Kwanza, natumai itawapa wasomaji mwangaza juu ya lugha ya washairi - mwangaza utakaowafaa katika usomaji wa mashairi. Pili, natumai makala itawapa mwongozo wale ambao wana hamu ya kutunga mashairi bali hawajui mizungu ya kupitia. Endapo mambo hayo mawili yatasibu, moyo wangu utaridhika. Itakuwa ni fahari kubwa sana kwangu kama mshairi kuona watu wakisoma mashairi

kwa hiari yao wenyewe kwani wanayaelewa na kuyafurahia badala ya kuwa wanayasoma kutokana na sharuti za mitihani. Pia kuzuka kwa washairi wengi kutakuwa ni jambo la manufaa makubwa kwa fasihi ya Kiswahili na vilevile hatua azizi katika maendeleo ya utamaduni wetu.

TANBIHI

1. Mbinu nyingi za utunzi nitakazozungumzia humu zinatumiwa sio tu katika ushairi pekee bali pia katika tanzu nyingine za fasihi. Hata hivyo, katika makala hii nitaongelea hizo katika muktadha wa shairi pekee.
2. Mifano yote ya ushairi wa Muyaka iliyomo humu imeondolewa kutoka M. H. Abdulaziz (1979): *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry*.
3. Wimbo huu umechapishwa katika J. Knappert (1979). Katika kitabu hicho Knappert anasema kwamba wimbo huo huimbwa huko Mombasa.
4. Wimbo huu umechapishwa katika J. Knappert (1979). Katika kitabu hicho Knappert anadai kwamba wimbo huo huimbwa huko Siu.
5. Ni hatia kudondoa au kunukuu maandishi ya watu wengine bila kuonyesha wazi wazi kwamba unafanya hivyo. Hilo ni jambo la kutahadhari kwalo kwa wale ambao watavutiwa na kunga ya tadmini.
6. Kwa mujibu wa M. H. Abdulaziz (1979:88) mkarara wa beti hizo unatokana na Quran.
7. Akiongelea ubeti huo M. H. Abdulaziz (1979:137) anadai kwaba kiarabu kina methali inayosema “Al duny jif la yuhibhuhu ila I kilabu” yaani dunia ni mzog huvutia majibwa peke yao.
8. Kutoka shairi liitwalo ‘Nakumbuka ulivyokuwa’ lililomo katika diwani yangu ya *Radio na Mwezi*.
9. Miongoni mwa washairi wanaotumia imani za jamii katika ushairi wao ni Wole Soyinka. Kwa mfano, katika shairi lake refu liitwalo ‘Ogun Abibiman’, Ogun ambaye anaaminika kuwa:

Mungu wa Vita na Ubunifu, wa

Madini, wa Njia, Mrejezi wa Haki (tafsihi yangu)

ametumiwa. Pia katika shairi hilohilo mwandishi ametumia ‘Idanre’, kilima cha majabali katika eneo la Yoruba, Nigeria, ambapo anaaminika anaishi Ogun. Vilevile, jina “Ogun” limetumika katika shairi lake liitwalo ‘Idanre’ lililomo katika diwani yake ya *Idanre and other Poems*.

MAREJEO

1. Abdala, A. (1973) *Sauti ya Dhiki*; Nairobi: Oxford University Press.
2. Abdulaziz, M. H. (1979) *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
3. Abedi, K. (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: Kenya Literature Bureau (Toleo la 1979).
4. Hussein, E. (1976) *Jogoo Kijijini: Ngao ya Jadi*. Dar es Salaam: Oxford University Press
5. Kezilahal E. (1974) *Kichomi*. Nairobi: Heinemann Educational Books.
6. Knappert, J. (1979) *Four Centuries of Swahili Verse*. Nairobi: Heinemann Educational Books
7. Mayoka, J. M. (1984) *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
8. Wa Mberia, K. *Rangi za Ushairi*. Mswada
9. Wa Mlamali, M. (1980) *Inkishafi: Ikisiri ya Muhamadi wa Mlamali*: Nairobi: Longman Kenya

10. Mohamed, A. (1980) *Sikate Tamaa*.
11. Mulodozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979): *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*.
12. wa Muti K. (1982) *Uhakika wa Malenga wa Mvita*. Tasnifu ya
B. A., Chuo Kikuu cha Nairobi.
13. Nassir, A. (1971) *Malenga wa Mvita: Diwani ya Ustadh*
Bhalo. Nairobi: Oxford University Press
14. Soyinka, (1987) *Idanre and Other Poems*. London: Nethuen
& Co.Ltd
15. _____ (1976) *Ogun Abibiman*. London: Rex Collings
Ltd/Ibadan: Open Ifa.
16. TUKI (19 84) “Msamiati wa Muda wa Fasihi” Katika
Mulika na 16. Dar-es-Salaam. Taasisi ya
Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha
Dar-es-Salaam

Makala hii iliwasilishwa katika Semina ya Walimu, Idara ya Ismu na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Nairobi, mnamo 1987.